HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA | TOLEO LA 003 | SEPTEMBA 2024 | HALIUZWI

# CHUNYA

Jarida la Mtandaoni

## ZAWADI YETU




**MHARIRI MKUU**
TAMIM H. KAMBONA
Mkurugenzi Mtendaji wilaya ya Chunya

**MHARIRI MSAIDIZI**
JOSHUA. A. SENGO
Kaimu Mkuu wa kitengo cha Habari Wilaya ya Chunya
SELEMANI SHEKONGA
Afisa Habari-Wilaya ya

**WAPIGA PICHA**
JOSHUA A. SENGO
FATUMA MTWEVE
SELEMANI SHEKONGA

**MSANIFU WA JARIDA**
FATUMA MTWEVE
Afisa Habari-Wilaya ya Chunya

# UONGOZI WA WILAYA YA CHUNYA




Mhe. Mbarak Alhaji Batenga
Mkuu wa wilaya ya Chunya



Mhe. Bosco Mwanginde
Mwenyekiti H/Shauri ya Chunya



Mhe. Masache Njelu Kasaka
Mbunge Jimbo la Lupa



Ndugu; Anakleth Michombero
Katibu tawala wilaya ya Chunya



Ndugu; Tamim Kambona
Mkurugenzi Mtendaji - Chunya

# MKOA WA MBEYA UNAJIVUNIA WILAYA YA CHUNYA; MATUMIZI MAZURI YA MAPATO YA NDANI



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Zuberi Homera amesema Mkoa wa Mbeya unajivunia Halmashauri ya wilaya ya Chunya katika matumizi mazuri ya Mapato ya Ndani Jambo linalopelekea Halmashauri hiyo kutekeleza miradi mikubwa, mizuri na yenye lengo la kuwasogezea huduma wananchi wake na kwakufanya hivyo Chunya wanakuwa wametafsiri vyema lengo na nia thabiti ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassani.

Mhe Homera alitoa kauli hiyo mapema Septemba 9, 2024 wakati wa Hafla ya utiaji saini Mkataba wa Ujenzi wa Stendi Mpya ya Mabasi wilayani Chunya ambayo inataraji kujengwa kijiji cha Sinjilili ndani ya kata ya Itewe

"Tunajivunia Wilaya ya Chunya kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani na matumizi sahihi ya mapato hayo kwani mmejenga miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri." alisema Homera.

Aidha, Homera aliwataka wananchi wa wilaya ya Chunya kuendelea kuinga mkono Serikali iliyoka madarakani ili ujenzi wa Miundombinu mbalimbali inayoendelea kujengwa Chunya iendelee na ikamilike kwa wakati jambo ambalo litaendelea kuipa heshima Chuna na Mkoa kwa ujumla

Naye Mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe. Mbaraka Alhaji Batenga amemhakikishia mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwamba watasimamia ujenzi wa stendi hiyo ya mabasi inayotarajiwa kuanza kujengwa mapema mwezi septemba ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati uliokusudiwa na kwa viwango ili wananchi wa wilaya ya Chunya waanze kunufaika na Stendi hiyo mapema.

Aidha , Mhe. Batenga amesema Wilaya ya Chunya ni Wilaya ya madude (majengo) na wananchi wake wamekuwa wakijituma na kuchangia shughuli mbalimbali za Maendeleo ili kuungana na Serikali kuhakikisha wananchi wake wakiwepo wananchi wa wilaya ya Chunya wanapata Mendeleo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya, Mhe. Bosco Mwanginde wakati akitoa salamu

za wananchi kwa Mkuu wa mkoa amesema yeye na baraza la Madiwani kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya watahakikisha wanasimamia ujenzi huo kwa weledi na kuhakikisha muda waliokubaliana na mkandarasi kukamilisha ujenzi unazingatiwa na mradi unakamilika kwa viwango vilivopo kwenye mkataba.

Awali akitoa taarifa ya ujenzi wa stendi hiyo ya mabasi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ndugu Tamimu Kambona amesema ujenzi wa Stendi ya Mabasi Chunya ni utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipofanya ziara yake Chunya mwaka 2022, na ameongeza kuwa mradi huo utagharimu kiasi cha Bilion 3.1 ambazo ni mapato ya ndani ya Halmashauri.






“Stendi hii ni maagizo ya Mheshimiwa Rais alipokuja Chunya mwaka 2022, aliagiza Halmashauri ijenge stendi kupitia mapato yake ya ndani na sisi tumanza kutekeleza agizo hilo na utekelezaji wake utachukua miezi tisa” alisema Kambona.

Hafla ya kusaini Mkataba wa ujenzi wa Stend mpya ya Mabasi Chunya imefanyika tarehe 9/9/2024 katika viwanja ambapo stendi hiyo inajengwa na mkandarasi mzawa ambaye ni AMJ Global Mult Constractors Company na itajengwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

# RC CHONGOLO, MAONESHO YA NANENANE NI KWAAJILI YA KUJIFUNZA



Mkuu wa mkoa wa songwe Mhe. Daniel Chongolo amesema kuwa lengo la kutembelea Maonesho ya nanenane ni pamoja na kujionea na kujifunza namna ambavyo technolojia inafanyakazi katika sekta ya kilimo na mifugo na kuweza kuleta tija kwa wakulima na wafugaji katika uzalishaji kwajili ya kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Chongolo ameyasema hayo alipotembelea banda la Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwaajili ya kujione na kujifunza mambo mbalimbali yanayopatikana katika banda hilo kwenye maonesho ya nanenene Nyanda za juu kusini katika viwanja vya John Mwakangale Mkoa wa Mbeya.

“Kwenye maonyesho haya sisi tunapita kwanza kujifunza lakini pia kujionea namna ambavyo technologia iliyoboreshwa inavyoendelea kufanya kazi kwenye maeneo ya kilimo , uvuvi na ufugaji kwaajili ya kuongeza tija kwa wananchi”aliseme Chongolo

Aidha Mhe .Chongolo ametembelea kujifunza na kujionea bidhaa za kilimo ikiwa ni pamoja na mbegu za mazao mbalimbali, mazao ya misitu ikiwemo asali, masalia ya wanyama pori kama vile ngozi ya mamba, fuvu la kichwa cha tembo, viatu vya ngozi pamoja na makundi mbambali ya vyakula pamoja na vichangamshi kwaajili ya watoto na mambo mengine mengi.

Mkuu wa mkoa wa Songwe ametembelea mabanda mbalimbali katika maonyesho ya nanenane nyanda za juu kusini ikiwa ni siku ya sita (6) tangu maonyesho hayo yalipoanza tarehe 1 Agosti yanayotaraji kuhitimishwa tarehe 8 Agosti mwaka huu.



## WAKUU WA IDARA NA VITENGO WAHIMIZWA KUTIMIZA AHADI ZAO KUCHANGIA UJENZI WA UWANJA



Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya ameongoza kikao cha wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya kufanya kikao hicho kwenye uwanja ambao unaendelea kujengwa ikiwa ni kuwahimiza kutimiza ahadi zao walizo ahidi wakati wa Harambee ya kuchangia ujenzi huo iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ili lengo la Serikali ya kukamilisha ujenzi wa uwanja huo limitime mwaka huu wa fedha 2024/2025

Kikao hicho kilichofanyika leo tarehe 01/07/2024 kwenye uwanja wa Michezo unaojengwa wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya ili kuanza Mwaka mpya kwa kasi na kuonesha dhamira ya Serikali kukamilisha ujenzi wa uwanja huo mapema ili wananchi wa wilaya ya Chunya na watu wengine kutoka nje ya wilaya ya Chunya waanze kuja kupata burudani mbalimbali kupitia kukamilika uwanja huo

Kupitia kikao hicho wajumbe wamekubaliana kuundwa kwa kamati ya kukusanya micho itawatakiwa kupita kila kata ili kuhimiza wananchi wa Chunya kushiriki kuchangia uwanja wao jambo ambalo litaharakisha kukamilisha kazi ya ujenzi wa uwanaj huo ili wananchi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya waanze kupata burudani mbalimbali kupia uwepo wa uwanja huo huku fursa mbalimbali za kiuchumi zikiendelea kufunguka kupitia uwepo wa uwanja huo

Ikumbwe Halmashauri ya wilaya ya Chunya inajenga uwanja wa Michezo unaojumuisha viwanja vya michezo mbalimbali, Ujenzi wa uwanja huo uko hatua mbalimbali huku jingo la kubadirishia nguo likiwa Zaidi ya asilimia 85, ukuta umekamilika kwa asilimia 60, eneo la kuchezea liko karibu asilimia 40 na kazi inaendelea

Aidha ikumbukwe pia Timu ya KenGold kutoka wilaya ya Chunya imefanikiwa kupanda Daraja hivyo msimu wa 2025/2024 itacheza ligi kuu, na ni matumaini ya Serikali kukamilika kwa uwanja huu utaongeza hamasa kwa vijana kuona fursa kwenye michezo lakini wananchi wa wilaya ya Chunya kupata fursa mbalimbali za kiuchumi

# KAMPUNI YA PREMIUM KUFADHILI WATAKAOPATA DARAJA LA KWANZA KIDATO CHA NNE 2024 KIPEMBAWE



Naye Bi Delister Hyera Mkuu wa kitengo cha TEHEMA kutoka Kampuni ya ununuzi wa Tumbaku ya PREMIUM amesema Kampuni yake itagharimia masomo ya Shule ya Upili (A' Level) wanafunzi wawili watakaofanya vizuri masomo yao kwa kupata daraja la kwanza katika mtihani wao wa kidato cha nne mwaka 2024.

"Si mmeniahidi mtafaulu vizuri? Sasa na mimi natoa zawadi kwa kaka mmoja na dada mmoja atakayepata daraja la kwanza (Division one) tutalipia ada kwa kidato cha tano na kidato cha sita lakini na mimi nitakuwa na zawadi yangu binafsi kwa mdada atakayefanya vizuri, nitamshonea sare za Shule (uniform) kokote anatakokwenda kusoma masomo yake ya 'A level' niwaombe mtunze ahadi hizo" Amesema Bi Hyera

Awali akiwasilisha mada yake Afisa tarafa wa Tarafa ya Kipembawe ndugu Kassim Kirondomara amesema namna pekee ya kubadiri ugumu wa Maisha wanaokabiliana nao wazazi wa wanafunzi walioko Shuleni hasa wale wa Kidato cha nne 2024 ni kusoma kwa bidii ili wafaulu mtihani waon hatimaye waendelee na masomo ya Juuu.

"Matokeo yenu ya mwaka jana yalikuwa sio ya kuridhisha kabisaa kwani zaidi ya asilimi 80 ya wanafunzi walimefeli, na matokeo yenu ya mtihani uliofanyika mwezi mei hayaakisi malengo ya wilaya yetu na mkoa wetu na hata upande wenu hayawapeleki kokote ambapo wanafunzi zaidi ya mia moja wamepata daraja la nne na daraja sifuli huku wanafunzi watatu tu wakiwa wamepata daraja la tatu, hakuna daraja la pili na hakuna daraja la kwanza, Nimeumia sana." Alisema Kirondomara

Aidha Kirondomara alimekumbusha wanafunzi juu ya Shughuli kuu ya uzalishaji mali inayofanywa na wazazi wa wanafunzi wengi Tarafa




ya Kipembawe kwamba ni kilimo cha Tumbaku kwa kusisitiza ugumu wa kazi hiyo amewataka wanafunzi kuongeza bidii sana katika maandalizi ya mitihani yao ili baadaye waweze kuzikomboa familia zao.

"Nimeambiwa hapa kwamba mmemaliza mada zote katika masomo yote, na nimeambiwa mmefanya mtihani wa Kanda matokeo yake yataletwa hivi karibuni, nitafurahi kuona matokeo yanabadirika ukilinganisha na yale ya awali na tuanze kuondoa ziro kwani wewe unayepata ziro maana yake unafanana na mtu ambaye hajasoma kabisa. Niwakumbushe Wazazi wenu wanafanya kazi Ngumu sana ili kuhakikisha wewe unasoma na unafikia malengo yako na wewe ndiye unatarajiwa kubadirisha maisha magumu ya familia yako nyumbani na namna sahihi ya kufanikisha hilo ni kufaulu mitihani yako ili uende hatua nyingine za kielimu" aliendelea kuongeza Kirondomara

Baada ya mawasilisho mbalimbali kutamatika wanafunzi wakiongozwa na Afisa Tarafa wa tarafa ya Kipembawe wamekula kiapo ya kuhakikisha wanapata daraja la kwanza, daraja la pili na daraja la tatu, huku kipo hicho kikieleza hakuna mwanafunzi atakayepata daraja la nne na daraja sifuri

"Sisi wanafunzi wa Kidato cha Nnne (wakitaja Shule zao) tunaahidi ya kwamba hatupata daraja Sifuli wala daraja la nne, mtu atakaye feli atapata daraja la tatu, wengine tuliobaki tutapata daraja la pili na daraja la kwanza. Tunaahidi kwako afisa tarafa na viongozi meza kuu wote. Na tuaahidi kwa wazazi wetu walioko Nyumbani kwamba tunapata daraja la kwanza mpaka daraja la tatu ili tuweze kuenda kidato cha tano. EEE Mwenyeezi MUNGU tusaidie"

Afisa tarafa wa tarafa ya Kipembawe Ndugu Kassim Kirondomara yuko kwenye ziara ya kuhamasisha wanafunzi kusoma kwa bidii ili kufika hatma njema ya Maisha yao ili hapo baadaye waweze kukomboa familia zao kutoka katika hali duni. Katika Ziara hiyo amekuwa akiongozana na wadau mbalimbali wakiwepo Kampuni za ununuzi wa Tumbaku, viongozi wa Serikali na wadau wengine



# CHUNYA YAENDELEA KUTAFUTA MWAROBAINI WA KULINDA WANYAMAPORI, VIUMBE HAI NA KUZUIA UHARIBIFU WA MAZINGIRA




Shirika la TDFT chini ya mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili kwa ufadhiri wa watu wa Marekani wamefanikisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi sitini (60) wa Shule za Msingi na Sekondari zenye kutoka tarafa ya Kipembawe wilayani Chunya zenye Klabu za Uhifadhi wa wanyama pori, viumbe hai na utunzaji wa mazingira kwa ujumla (TAWA MALIAHAI KLABU) kwenda kujifunza uhifadhi wa wanyamapori, viumbe hai na utunzaji wa Mazingira katika hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Akifafanua kuhusu ziara hiyo meneja wa mradi Ndugu Samson Ipyana Mwakihaba amesema lengo la ziara hiyo ni kuwafundisha kwa vitendo wanafunzi wanachama wa klabu za uhifadhi wanyama pori, viumbe hai na utunzaji wa Mazingira kwa ujumla ili kwanza kuthibitisha walichojifunza kwa nadharia lakini pia kuongeza uelewa juu ya uhifadhi, na baadaye kuandaa mabalozi sahihi na wenye uelewa sahihi wa uhifadhi wa wanyama pori, viumbe hai na utunzaji wa mazingira kwa ujumla wake

"Tuko kwenye ziara kwa lengo la kuongeza elimu kwa vitendo juu ya Uhifadhi wanyapori, viumbe hai na mazingira kwa ujumla huku Lengo likiwa ni kuandaa mabalozi wazuri wa uhifadhi wa wanyama pori, viumbe hai na utunzaji wa Mazingira kwa ujumla na bila shaka watakuwa walimu wazuri kwa watu wengine hususani jamii inayowazunguka hivyo lengo la kuongeza Elimu juu ya uhifadhi wa wanyamapori, viumbe hai na utunzaji wa mazingira litakuwa limefanikiwa" Amesema Mwakihaba

"Tuko kwenye ziara kwa lengo la kuongeza elimu kwa vitendo juu ya Uhifadhi wanyapori, viumbe hai na mazingira kwa ujumla huku Lengo likiwa ni kuandaa mabalozi wazuri wa uhifadhi wa wanyama pori, viumbe hai na utunzaji wa Mazingira kwa ujumla na bila shaka watakuwa walimu wazuri kwa watu wengine hususani jamii inayowazunguka hivyo lengo la kuongeza Elimu juu ya uhifadhi wa wanyamapori, viumbe hai na utunzaji wa mazingira litakuwa limefanikiwa" Amesema Mwakihaba




jiografia ya nchi yao hivyo kuendelea kukuza uzalendo ndani ya mioyo yao lakini inaongeza hamasa kwanza kwa washiriki wa safari na baadaye wanafunzi wengine nao watahamasika kushiriki kwenye uhifadhi wa mazingira wakijua iko siku nao wataenda kujifunza maeneo mengine mbali na nyumbani kwao

Aidha Mwakihaba pamoja na kuishukuru Serikali ya Marekani kufadhiri mradi huo uliopelekea wanafunzi kupata ziara ya mafunzo kwa vitendo, pia ametaja Shue zilizonufaika na ziara hiyo ya mafunzo Shule ya Sekondari Mtanila (wanafunzi 10), Shule ya Msingi Matwiga (Wanfaunzi 10) Shule ya Msingi Mafyeko (wanafunzi 10), Shue ya Msingi Bitimanyanga (wanafuzni 10), Shule ya Msingi Kambikatoto na Shule ya Msingi Sipa (wanafunzi 10) hivyo kukamilisha idadi ya wanafunzi 60. Walimu wane kutoka Sipa, Matwiga, Bitimnyanga na Mtanila waliungana ili kuwasimamia wanafunzi hao

Afisa kutoka idara ya Maendeleo ya Jamii wilaya ya Chunya ambaye alikuwa mmojawapo katika Safari hiyo Bi Jennifer Oscar amesema safari inafaida kubwa kwa Halmashauri ya wilaya ya Chunya kwani pamoja na kuongeza uelewa wa washiriki katika mambo ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira amesema wanafunzi wamepata burudani, wameongeza kuifahamu jiografia ya nchi yao hivyo kuendelea kukuza uzalendo ndani ya mioyo yao lakini inaongeza hamasa kwanza kwa washiriki wa safari na baadaye wanafunzi wengine nao watahamasika kushiriki kwenye uhifadhi

## CHUNYA YAJIPANGA KULIPA STAHIKI ZA WATUMISHI KWA WAKATI



Mbunge wa Jimbo la Lupa Mhe Masache Njeru Kasaka amewata viongozi wa Halmashauri kuhakikisha wanatumia vizuri vifungu vinavyotakiwa kulipa stahiki mbalimbali za watumishi kuepuka kuisha au kubasti kwa vifungu hivyo jambo linalopelekea Halmashauri kushindwa kuwalipa watumishi wake wanapohitaji kulipwa jambo linaloongeza madeni kwa Halmashauri.

Ametoa kauli hiyo mapema

tarehe 27/8/2024 wakati akitoa salamu kwenye kikao cha Baraza la Madiwani liloketi kujadili na kupitisha hesabu za mwisho wa mwaka 2023/2024 za Halmashauri ya wilaya ya Chunya kilichoketi kwenye ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri uliopo jingo jipya la utawala.

"Tunatakiwa kujipanga kuona vipengele vyakulipa madeni havibust na kuweza kulipa malipo mbalimbali" alisema Kasaka.

Aidha Mhe. Kasaka aliongeza kuwa mambo mazuri yanayotokea ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya ni utekelezaji mzuri wa ilani ya Chama cha Mapinduzi huku akisema usimamizi mzuri wa Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na ushirikiano uliopo baina ya waheshimiwa Madiwani na Wataalam.

Pia Mhe Masae aliungana na kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za mitaa (LAAC) kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa maendeleo makubwa yaliyopo kwenye Wilaya hiyo.

"Mwanzoni wa mwezi Agosti, LAAC ilifanya kikao chake, pamoja na mambo mengine imeipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa kufanya vizuri kwenye ukusanya wa mapato na matumizi ya fedha za mapato hayo" alisema Kasaka.

Baraza la kujadili na kupitisha hesabu za mwisho za mwaka 2023/2024 za Halmashauri limehudhuriwa na Mkuu wa Wilaya, Mbunge, Waheshimiwa Madiwani, Wataalam mbalimbali kutoka Halmashaui



## DC BATENGA, WALIOVAMIA ENEO LA MRADI WA KILIMO CHA SOYA KIJIJI CHA MASIANO CHUNYA WAONDOKE



DC Batenga amewataka wananchi wa kijiji cha Masiano kuheshimu mpango bora wa matumizi ya ardhi ambao umepitishwa na wananchi hao kupitia mikutano yao ya kijiji ili kuondoa migogoro ya ardhi pamoja na kuwataka wananchi hao kuisha kwenye eneo moja ili Serikali iweze kuleta huduma na maendeleo kwenye makazi yao.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mheshimiwa Mubarak Alhaji Batenga amewataka wananchi wa kijiji cha Masiano wilayani Chunya waliovamia eneo la mradi la kilimo cha Soya kuondoka kwenye eneo hilo mara moja ili kupisha utekelezaji wa mradi wa kilimo cha zao la Soya utakaotekelezwa na serikali hivi punde kupitia udhamini wa benki ya dunia.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara kijiji cha Masiano, Septemba 19, 2024, Mheshimiwa Batenga amesema wananchi wote waliovamia eneo la mradi wa kilimo cha Soya katika kijiji cha Masiano kilichopo Wilayani Chunya kuondoka .

"Waliovamia eneo la mradi wanapaswa kuondoka na Serikali itawapa kila kaya heka 50 pamoja na hati miliki katika eneo lililopo msitu wa kijiji ili kupisha utekelezaji wa mradi huu mkubwa wa kilimo cha Soya", amesema Batenga.

Mhe. Batenga aliongeza kuwa, wananchi wa Masiaono na Mapogolo ndio wanufaika wa kwanza mara baada ya mradi wa kilimo cha Soya kuanza kutekelezwa huku akiwataka vijana kujipanga vyema kushiriki kwenye mradi huo ili kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi.

Katika hatua nyingine, Mhe. Batenga amesema kupitia mpango bora wa matumizi ya ardhi, Serikali imetenga eneo lenye ekari 2594 lililopo kijiji cha Mapogolo na Shoga kwaajili ya wafugaji wa Kijiji cha Masiano na Mapogolo ambapo Serikali itapanda majani kwaajili ya malisho, kuchimba mabwawa ya



maji upatikanaji na kujenga majosho ya mifugo.
"Wananchi wa kijiji cha Masiano munapaswa kuheshimu mpango bora wa matumizi ya ardhi ambao mumeupitisha kupitia mikutano yenu ya kijiji na mpango huu mumeuhuisha kulingana na mahitaji yaliyopo sasa, kuwa na matumizi bora ya ardhi kutaondoa migogoro ya ardhi pamoja na serikali kuweza kuwaletea wananchi maendeleo" amesema DC Batenga.
Kwa upande wa wananchi wa kijiji cha Masiano walimueleza Mhe. Batenga changamoto zilizopo kwenye kijiji chao ikiwemo ubovu wa barabara, kutokukamilika kwa madarasa ya shule na upungufu wa madawati, ukosefu wa nishati ya umeme, upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kutokuwepo kwa zahanati kwenye kijiji hicho ambapo serikali imeahidi mwaka huu wa fedha kuzipatia ufumbuzi wa haraka.
Mhe. Batenga yupo kwenye ziara yake ya kawaida ya kukutana na wananchi kwa kila kijiji kusikiliza kero zao na kutatua. Wakati wa mkutano huu Mhe. Batenga amewakikishia wananchi kuwa kazi ya Serikali ni kutengeneza mazingira wezeshi kwa wananchi wake kujipatia kipato na kujikwamua kiuchumi, mradi wa kilimo cha Soya utakapoanza, Serikali itapeleka huduma zote muhimu za kijamii ikiwemo kuchonga barabara, huduma ya umeme na maji, kujenga zahanati, kujenga shule na huduma nyingine zote za kijamii.



"Wananchi wa kijiji cha Masiano munapaswa kuheshimu mpango bora wa matumizi ya ardhi ambao mumeupitisha kupitia mikutano yenu ya kijiji na mpango huu mumeuhuisha kulingana na mahitaji yaliyopo sasa, kuwa na matumizi bora ya ardhi kutaondoa migogoro ya ardhi pamoja na serikali kuweza kuwaletea wananchi maendeleo" amesema Batenga.

## KASANGA KANYIKA KUNUFAIKA NA HUDUMA YA MAWASILIANO MASAA 24



Wakazi wa kitongoji cha Kasangakanyika kilichopo kijiji cha Lupa maketi katika kata ya Ifumbo wanakwenda kuondokana na changamoto ya mawasiliano kupitia ujenzi wa mnara wa mawasiliano unaojengwa katika Mlima Igalawa uliopo katika kitongoji hicho hali itakayo rahisisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano muda wote.
Hayo yamezungumzwa na Mbunge wa Jimbo la Lupa Mhe. Masache Njelu Kasaka wakati akizungumza na kusikiliza kero za wananchi katika kitongoji cha Kasangakanyika kilichopo kijiji cha Lupamaketi Kata ya Ifumbo Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.
"Maisha ya sasa hivi ni maisha ya mawasiliano ya simu za mkononi usipokuwa na mawasiliano unakuwa umepoteza fursa mbalimbali ambazo ungeweza kuzipata .Tunaendelea kuboresha hilo



na ninavoongea na ninyi hapa tunakwenda kuwajenga mnara hapa katika Mlima Igalawa na vifaa tayali vimeshaletwa vipo kwenye ofisi ya Mtendaji wa kata ili kuwa na uhakika wa mawasiliano hapa masaa ishirini nan ne(24)"alisema Mhe. Masache.

Aidha Mhe.Masache amewapongeza wanachi na wadau wa kitongoji cha KasangaKanyika kwakwendelea kujitoa kwa hali na mali katika ujenzi wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kunza ujenzi wa Shule ambapo ameahidi kuwaunga mkono kwa kuwachangia mifuko hamsini (50) ya saruji ili iweze kuwasaidia ujenzi huo .

Atupakisye Mwansembo mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa niaba ya Wananchi wengine ampongeza Mhe. Masache kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwaletea maendeleo wananchi wake wa Kitongoji cha Kasangakanyika na kata ya Ifumbo kwa ujumla na kuomba utekelezaji kwa mambo mbalimbali ambayo Wananchi wameyaomba .

"Sisi tunakupongeza pamoja na kamati zako kutoka Wilaya na kata kwasababu maendeleo tunayaona ,tunakuomba twendelee kushirikiana pamoja na wewe ili vitu hivi vikamilike kwasababu tukianza kwa moto tukarudi kuwa baridi tutakuwa hatujafanya chochote , usijiulize kwanini niko hapa mama wa CHADEMA ni kwasababu Malaria bila Mseto haijapona bado sisi tuko pamoja na wewe tunachotaka ni viongozi bora na sio bora viongozi"alisema Atupakisye.

Ziara ya Mhe. Mbunge ya kuzungumza na kutatua kero mbalimbali za wananchi imefanyika katika ngazi za Vitongoji ikijumuisha viongozi wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Wilaya , kata, kijiji na kitongoji pamoja Wanachi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.



# VIJANA SASA KUWEZESHWA KUCHIMBA DHAHABU CHUNYA



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 ndugu Godfrey Eliakimu Mnzava amekabidhi leseni 11 za uchimbaji madini kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chunya ndugu Tamim Kambona kwaajili ya kuwezesha Vijana kuchimba Madini kwa vitalu vyenye ukubwa wa ekari 151.8 vyenye gharama ya zaidi ya millioni sita vilivyopo msitu wa hifadhi wa Mbiwe kata ya Matundasi.

Akizungumza kwenye Mkesha wa Mwenge wa uhuru uliofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Makongolosi Agosti 24 mwaka huu, Mzava alisema kuwapatia leseni wachimbaji wadogo ni kurasimisha na kuongeza mnyororo wa thamani kwa vijana walioamua kujiajiri kupitia sekta hii ya madini.

"Ninyi viongozi wetu wa Wilaya mmetafsiri maono ya Mhe. Rais kwa vitendo kwa kuwapatia leseni kundi hili la vijana ili waweze kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli ya uchimbaji na hii ndio dhana ya uwezeshaji Vijana kiuchumi" alisema Mnzava.

Mzava aliwahimiza Viongozi wa Wilaya kuwawezesha mitaji wachimbaji wadogo kupitia kundi la vijana ili kuongeza mnyororo wa thamani kwenye sekta ya madini



ambayo ni chanzo kimojawapo cha kuingiza mapato kwenye Wilaya hiyo.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya jamii, Bi Marietha Mlozi akisoma taarifa ya mpango maalum wa urasimishaji wa wachimbaji wa dogo katika sekta ya madini kwenye sherehe za Mwenge alisema, vijana watapata manufaa mbalimbali ikiwemo kujiajiri na kuweza kuajiri vijana wengine na kujiongezea kipato.

"Kupitia Programu maalum ya urasimishaji kwa wachimbaji wadogo kutawawezesha vijana hawa kunufaika moja kwa moja na rasirimali za Taifa na kuwezesha kuwa na maeneo ya uhakika ya uchimbaji wa madini" alisema Mlozi

Mlozi aliongeza kuwa, mpango wa urasimishaji kwa wachimbaj utawawezesha kupata mikopo ya riba nafuu pamoja na kujitegemea kufanya shughuli hii ya uchimbaji kwa ufanisi.

Mwenge wa Uhuru Wilaya ya Chunya umekimbizwa umbali wa kilometa 287.4 na miradi mbalimbali yenye thamani ya shilingi

## CHUNYA WAONYWA KUNUNUA DAWA KWENYE MAENEO YASIYO RASMI




Mamla ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imewaonya wananchi wa wilaya ya Chunya kununua Dawa kwenye maeneo yasio rasmi na kununua dawa bila kupata ushauri wa kidaktari jambo ambalo husababisha usugu wa wadudu wa homa katika miili yao wakiendelea kununudua dawa za binadamu au dawa za mifugo bila kuzingatia maeneo yanayouza dawa hizo na wakiendelea kununua dawa bila kufuata ushauri wa wataalamu wanahatarisha afya zao wenyewe na afya za mifugo yao

Katika nyakati tofauti wakaguzi wa dawa kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba Bwana Selemani Mayala na Bi Grace Kapande wametumia muda mwingi kutoa elimu ya Matumizi sahihi ya dawa kwa binadamu na mifugo na kwakufanya hivyo wataimarisha afya za wananchi wenyewe na mifugo yao jambo litakalopelekea lengo la Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na he Dkt Samia Suluhu Hassan linatimia kwa wananchi kuwa na Afya njema

Aidha Seleman amesema Lengo la Serikali kuajiri maafisa Mifugo wengi na kupangwa kwenye kata na vijiji mbalimbali nchi ni kurahisisha na kuhakikisha wafugaji wanapata huduma kwa haraka na kwa urahisi Zaidi jambo litakalopelekea mifugo yao kuwa na afya wakati wote hivyo kuepelea ongezeko la kipato kwa wananchi wafugaji na hata kulinda usalama wa wananchi wanatumia mazo ya mifugo kama Maziwa na Nyama

"Kila kata ina madaktari wa Mifugi, Serikali imeamua kuweka madaktari wa mifugo kwa kila kata ili kuwasaidia wafugaji ili mifugo itibiwe kwa fuata maelekezo ya wataalamu. Ukiona ngombe wako afya yake ina badirika, ngombe amekuwa a teza




Mamla ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imewaonya wananchi wa wilaya ya Chunya kununua Dawa kwenye maeneo yasio rasmi na kununua dawa bila kupata ushauri wa kidaktari jambo ambalo husababisha usugu wa wadudu wa homa katika miili yao wakiendelea kununudua dawa za binadamu au dawa za mifugo bila kuzingatia maeneo yanayouza dawa hizo na wakiendelea kununua dawa bila kufuata ushauri wa wataalamu wanahatarisha afya zao wenyewe na afya za mifugo yao

Katika nyakati tofauti wakaguzi wa dawa kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba Bwana Selemani Mayala na Bi Grace Kapande wametumia muda mwingi kutoa elimu ya Matumizi sahihi ya dawa kwa binadamu na mifugo na kwakufanya hivyo wataimarisha afya za wananchi wenyewe na mifugo yao jambo litakalopelekea lengo la Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na he Dkt Samia Suluhu Hassan linatimia kwa wananchi kuwa na Afya njema

Aidha Seleman amesema Lengo la Serikali kuajiri maafisa Mifugo wengi na kupangwa kwenye kata na vijiji mbalimbali nchi ni kurahisisha na kuhakikisha wafugaji wanapata huduma kwa haraka na kwa urahisi Zaidi jambo litakalopelekea mifugo yao kuwa na afya wakati wote hivyo kuepelea ongezeko la kipato kwa wananchi wafugaji na hata kulinda usalama wa wananchi wanatumia mazo ya mifugo kama Maziwa na Nyama

"Kila kata ina madaktari wa Mifugi, Serikali imeamua kuweka madaktari wa mifugo kwa kila kata ili kuwasaidia wafugaji ili mifugo itibiwe kwa fuata maelekezo ya wataalamu. Ukiona ngombe wako afya yake ina badirika, ngombe amekuwa mnyonge, amelegea wewe usimtibu kwasababu wewe haujui mgonjwa unaomsumbua huyo ngombe bali wasiliana na madaktari waliopo kwenye maeneo yetu" Alisema Seleman

Amewataka wafugaji kuzingatia mazingira ya uhifadhi wa dawa kwani dawa zozote ambazo zimehifadhiwa vibaya hupoteza uwezo wake wa kutIbu hivyo dawa hizo hazitasaidia wewe kama ni dawa za

binadamu na pia mifugo wako kwa dawa za mifugo kupona magonjwa hivyo amewataka wananchi kutonunua dawa maeneo yasiyo rasmi kinyume chake unahatarisha mifugo wako

"Daktari wa mifugo anajua ampe Ng'ombe dawa gani kulingana na hali aliyoiona, ninachoweza kukushauri usinunue dawa kiholela na nina uhakika ukinunua dawa kiholela unaenda kumtibu ngombe wako kuholela hole na kwakufanya hivyo ng'ombe wako hawatapona, atakuwa anatembea na wadudu na hatimaye wadudu wa ugonjwa huo watakuwa sugu na ngombe wako hawezi kuwa na afya nzuri na hata ukimleta hapa sokoni atakosa soko" Alisema Selemani wakati akitoa Elimu kwenye mnada wa Mapogolo Chunya

Awali akitoa utangulizi na ufafanuzi kuhusu Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA) afisa Elimu kwa umma wa Mamla ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA) Bi Maria Sanga amesema Lengo la Serikali kuanzisha mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba ni kulinda afya za jamii ya watanzania wakiwepo wananchi wa wilaya ya Chunya na kutekeleza hilo Serikali imewatuma kutoa elimu ya utumiaji mzuri wa dawa kwa wananchi wa Chunya na maeneo mengine

"TMDA ilianzishwa kwaajili ya kusimamia madawa ya binadamu na mifugo, vitendanishi, ilianzishwa kwaajili ya kusimamia tumbaku na mazalia yake lengo lengo kuu ni kulinda afya za jamii ili watumiaji wasipate madhara yoyote ndo lengo la Serikali kuanzisha mamla hii, Changamoto kubwa inakuja kwa sisi watumiaji wa mwisho, wengi tumekuwa tunatumia bidhaa hizi vibaya jambo libalopelekea kupoteza maisha na wengine kupata kupata madha mbalimbali ikiwepo kansa na mengine hivyo Serikali imetutuma kutoa elimu kwa wananchi ili tuondokane na usugu wa vimelea"

Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba imefanya ziara ya kutoa elimu kwa Umma ndani ya wilaya ya Chunya ambapo tarehe 4/09/2024 walikuwa kwenye mnada wa Mapogoro ambapo walizungumza na wafugaji na baadaye walizungumza na wafanyabiashara lakini kwa siku ya tarehe 5/9/2024 walitoa Elimu kwenye Kijiji cha Chalangwa na baadaye kitongoji cha Idendeluka

## TAKUKURU CHUNYA YAWAFIKIA WATUMISHI WA AFYA



Taasisi ya kuziua na kupambana na Rushwa TAKUKURU wilaya ya Chunya imewafikia waganga wafadhi  wa vituo vya Afya na zahanati zote zilizopo wilayani Chunya ili kutoa Elimu ya namna ambavyo wanaweza kuungana na Taasisi hiyo kuzuia na Kupambana na Rushwa jambo litakalopelekea wao kama watumishi wakawa salama lakini lengo la huduma bora kwa watanzania likatimizwa bila upendeleo.

Akizungumza wakati wa Mafunzo hayo leo tarehe 20/09/2024 kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri Afisa kutoka TAKUKURU wilaya ya Chunya Ndugu Gift Chihimba amewataka waganga wafawidhi kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na miongozo wanapowahudumia wananchi wao, kwa njia hiyo watakuwa wametekeleza majukumu yao vizuri lakini wanakuwa wamemsaidia Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupeleka Huduma stahiki kwa wanannchi wa Tanzania wakiwepo wananchi wa wilaya ya Chunya

Mganga Mkuu wa wilaya ya Chunya Dkt Darison Andrew amesema kikao hicho kinapaswa kufanyika kila robo ya mwaka kikilenga kufanya tathimini kwa ujumla ya hali ya Afya na kupitia kikao hicho ndipo maeneo ya kuongeza mkazo hudhihirika na kuwekewa mikakati na mipango ya pamoja.

"Kikao hiki kinapaswa kufanyika kila robo mwaka na lengo lake ni kufanya tathimini ya utoaji wa huduma kwa ujumla na tumewaalika TAKUKURU kwa lengo la kutoa elimu kwa watumishi hawa ili wawe na ufahamu wa mambo mbalimbali ya kufanya na mambo ambayo hayapaswi kufanya wakati wakiendelea kuwahudumia wananchi wa Chunya" amesema Dkt Darison

Pamoja na mafunzo hayo waganga wafawidhi wa vituo hivyo wamepaza sauti kutoka Elimu iendelee kutolewa ili wanaume (Wakina baba) Watambue umuhimu wa wao kuongozana na wenza wao kwenda vituo vya kutolea huduma ili kupata ushauri wa kidaktari pamoja na kwa kufanya hivyo dalili za Rushwa na upendeleo zitakuwa zimekomeshwa jambo ambalo litapunguza zaidi vifo vya Mama wajawaziti na watoto



"Wanaume hawaongozani na wenza wao kwenda vituo vya kutolea huduma kama utaratibu ulivyokuwa umetangazwa hapo awali na tunapochukua hatua ili angalau kuhimiza wanaume kuongoza/kuambata na wenza kuja kwenye vituo vya kutolea huduma tunaanza kunyooshewa vidole kwamba tunakiuka Sheria na taratibu za kazi sasa mnapokpata nafasi Elimu iendelee kutolewa juu ya umuhimu wa wanaume kuongozana na wenza wao" Amesema Febi Ambangile Kwa niaba ya waganga wafawidhi wengine Dkt Paul Saigod na Neema Mwafulilwa wamesema baadhi ya makosa yanatokana na mazingira yenyewe hivyo wamewaomba wasimamizi wa Sheria kutazama pande zote mbili wanaposimamia sheria hizo kuamua juu ya changamoto zinazokuwa zimejiokeza kwani wakati mwingine changamoto inajitokeza sio kwa makusudi.

Elimu ya Mapambano dhidi ya



# MHESHIMIWA BATENGA: CHUNYA KUKUSANYA BILIONI KUMI 2024/2025



Mkuu wa Wilaya ya Chunya Mhe. Mubarak Alhaji Batenga amesema kwa mwaka ujao wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Chunya ihakikishe inakusanya Bilioni 10 ili kuendana na kasi ya kuleta maendeleo kwenye Wilaya hiyo.

Batenga akihutubia kwenye Baraza la Madiwani liloketi kujadili na kupitisha hesabu za mwisho wa mwaka 2023/2024 za Halmashauri Agosti, 27 kwenye ukumbi wa Halmashauri alisema usimamizi mzuri wa ukusanyaji mapato ndio uliopelekea kuvuka lengo la kukusanya fedha nyingi zaidi ya makadirio waliojiwekea

"Mwaka wa fedha 2023/2024 tumevuka lengo la kukusanya mapato kwa asilimia 50, tumekusanya Billion 9, mwaka ujao ni Bilioni 10 tujipange vizuri kukusanya mapato hakuna kurudi nyuma" amesema Batenga.

Batenga ameipongeza Halmashauri kwa kuandaa taarifa nzuri ya hesabu za fedha, hoja zilizotolewa na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali zijibiwe zote vizuri ili wasivuke mwaka huu wa fedha wakiwa na viporo.

Pia Batenga aliongeza kuwa, Halmashauri inadaiwa zaidi ya Bilioni 2 ikiwemo madai ya watumishi, posho za safari, likizo na fedha za masomo nawahimiza kuangalia namna ya kulipa madeni haya ya watumishi ili kuongeza morali ya kufanya kazi kwa bidii.

"Watumishi walipwe kwa wakati kama ni vifungu vinaingiliana tuviangalie vizuri au tufanye reallocation, madeni haya yanapunguza morali ya kazi" amesema Batenga.

Halmashauri ikope kulingana na uwezo wake na ilipe madeni kwa wakati ili kuepuka riba kubwa kutoka kwa wanaowadai, alisisitiza Batenga.

Kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Batenga amesema, kuvuka malengo ya kukusanya mapato na uchangiaji wa asilimia arobaini kwenye miradi ya maendeleo ndio mrejesho mzuri na ndio uhalali wa kuendelea kuwepo madarakani kwa Chama cha Mapinduzi.

CCM imefanya kazi kubwa hakuna mahala utashindwa cha kueleza, Rais Sania amefanya zaidi ya walivyotarajiwa sasa ni mbele kwa mbele kuwaletea wananchi wetu maendeleo waliowaahidi wakati wa kuomba kura mwaka 2020.

"Tusiende kujiwekea miiba kwenye Uchaguzi huu wa serikali za mitaa tueleze maendeleo tuliyoafanya CCM, tueleze miradi tulioitekeleza na mengine tunayotarajia kuitekeleza" amesema Batenga.

Vilevile, Batenga aliwakumbusha watendaji wa Halmashauri kujipanga na kufanya maandalizi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na kuwapokea wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na shule ya awali, msingi na sekondari mwakani, 2025.

"Tunachotakiwa sasa ni kujipanga na majukumu yaliyo mbele yetu ikiwemo kuandaa miundombinu ya kuwapokea wanafunzi wa mwaka 2025 suala la madawati na uwiano wa wanafunzi na madarasa lakini pia uchaguzi wa serikali za mtaa tujipange vizuri" amesisita Batenga.

Tanzania inatarajia kufanya Uchaguzi wa serikali za mitaa kuchagua wenyeviti wa vitongoji Novemba 27 mwaka huu vilevile Uchaguzi mkuu unatarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka 2025 ambapo wananchi watachagua madiwani, wabunge na rais kuongoza nchi kwa miaka mitano ijayo.

## MIAKA MITATU YA MABADIRIKO CHUNYA: UKUSANYAJI WA MAPATO

| Mwaka | Makadirio | Makusanyo | Ziada/Pungufu<br>Ziada/Pungufu | Asilimia<br>% |
|---|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 5,579,554,407 | 5,391,820 | (187,733,496) | (3) |
| 2022/2023 | 5,271,510,965 | 5,998,238,458 | 726,817,493 | 14 |
| 2023/2024 | 6,543,358,000 | 9,850,753,349 | 3,307,395,349 | 50 |
| 2024/2025 | 8,747,616,00 | 1,514,531,932 | 7,233,084,067 | 17.31 |

Halmashauri ya wilaya ya Chunya imepiga hatua maeneo mbalimbali ya maendeleo ikiwepo eneo la uusanyaji wa mapato na kuyasimamia huku mabadiriki makubwa yakijitokeza kutoka kukusanya chini ya kiwango kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo walikusanya chini ya kiwango kwa asilimia tatu na kufikia kukusanya Zaidi ya asilimia mia moja na hamsini kwa mwaka 2023/2024

Katika vikao mbalimbali vya Halmashauri ya wilaya na hata vikao vya nje ya Halmashauri ya wilaya (Vikao vya Mkoa na vikao vinginevyo) Viongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya wametaja mambo mbalimbali yanayoipa nafasi Halmashauri kufanya vizuri maeneo mbalimbali ikiwepo eneo la ukusanyaji wa Mapato lakini kubwa kuliko sababu hizo ni Ushirikiano uliopo katika ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Ofisi ya Mbunge, Baraza la Madiwani pamoja na wataalamu wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Chunya Kupitia Ushirikiano huo kwa miaka mitatu mfululizo kuna mabadiriko makubwa ambapo kupitia mabadiriko hayo kwa sasa Chunya imeongezeka kiwango kutoka kupeleka asilimia

### OFISI YA MKUU WA MKOA MBEYA

**MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI ZA MKOA WA MBEYA KUANZIA TAREHE 01 JULAI 2023 HADI TAREHE 30 JUNI, 2024**

| Nafasi | Halmashauri | Makadirio ya Mwaka 2023/2024 | Hali ya Mapato ya ndani kufikia tarehe 30 Juni, 2024 | Asilimia iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Chunya DC | 6,543,358,000.00 | 9,802,892,149.50 | 150% |
| 2 | Busokelo DC | 2,000,000,000.00 | 2,674,048,354.42 | 134% |
| 3 | Kyela DC | 4,849,406,000.00 | 6,248,193,731.18 | 129% |
| 4 | Mbarali DC | 8,250,801,000.00 | 10,230,240,172.10 | 124% |
| 5 | Mbeya DC | 4,978,660,000.00 | 5,573,906,037.99 | 112% |
| 6 | Mbeya CC | 19,484,800,000.00 | 20,225,811,941.89 | 104% |
| 7 | Rungwe DC | 7,179,615,400.00 | 7,427,096,607.30 | 103% |
| **JUMLA KIMKOA** | | **53,286,640,400.00** | **62,182,188,994.38** | **117%** |

Chanzo: Halmashauri za Wilaya na Jiji Juni 30, 2024


arobaini (40%) ya makusanyo yake kwenye miradi ya maendeleo sasa kuanzia mwaka huu 2024/2025 Halmashauri ya wilaya ya Chunya itapaswa kupeleka asilimia sitini (60%) ya Makusanyo yake jambo ambalo litaendelea kuleta chachu katika utekelezaji wa miundombinu mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri hiyo

Jedwali la Makusanyo na mapato ndani ya miaka mitatu mfululizo

Mwaka Makadirio Makusanyo

Halmashauri ilikusanya chini ya kiwango kwa asilimia tatu(3 %)ambapo pesa pungufu kufikia malengo ilikuwa ni shilingi 187,733,496, Mwaka 2022/2023 Halmashauri ilikusanya Zaidi ya malengo iliyopangiwa kwa asilimia kumi na nne (14%) ambapo Halimashauri ilikusanya ziada ya shilingi 726,817,493, kwa mwaka 2023/2024 Halmashauri ilikusanya Zaidi ya malengo kwa asilimia hamsini (50%) ambapo pesa iliyokusanya ziada ya shilingi 3,307,395,349 Na Mwaka huu wa Fedha Halmashauri imekusanya shilingi 1,514,531,932 sawa na asilimia kumi na saba (17.31%).

Mabadiriko hayo kwa ujumla wake yanaleta athari Chanya kwenye utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwani miradi mingi Zaidi itatekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani kwani kwasasa Chunya itapeleka asilimia 60 ya mapato yake tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita ambapo Halmashauri ya wilaya ya Chunya ilikuwa inapeleka asilimia 40 ya mapato ya Ndani. Wananchi wa wilaya ya Chunya wategemee mabadiriko makubwa katika utekelezaji wa miradi




Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bwana Thobias Makoba amewataka maafisa Habari wa Mikoa na Halmashauri kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao ya kutoa taarifa za utekelezaji wa mambo mbalimbali yanayotekelezwa na Serikali katika maeneo yao ili wananchi wa Tanzania waendelee kufahamu namna Serikali yao inavyowajali akisistiza kwamba hilo ndilo jukumu lao la Msingi

Ametoa rai hiyo tarehe 3/08/2024 wakati wa kikao chake na maafisa habari wa Mikoa na Halmashauri kutoka Mikoa yaa Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe kilichoketi kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Eden Highland Mbeya kikiwa na lengo la kupokea changamoto zinazo wakumba na kuzitatua ili kuleta suluhu na hatimaye wananchi wapatiwe huduma wanazostahili kutoka kwenye kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kwenye Halmashauri na Mikoa yao




# Neo la Mhariri Mkuu

Kwanza niwapongeze wananchi wa Wilaya ya Chunya kwa namna mnavyoshiriki kwenye Shughuli mbalimbali za Maendeleo na kwa namna hiyo Tumeendelea kuijenga Wilaya ya Chunya kwa pamoja na kwa umoja na bila shaka Matokeo yanaonekana kila aliyepo Chunya na hata nje ya Chunya hapingi kwamba Chunya imebadirika sana

Pili, kutokana na tozo, ushuru na michango ya wadau Halmashauri imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ya kutolea huduma, niwaombe tuendelee kujitoa na kujituma kuhakikisha tunaungana na Mhe Rais kuhakikisha wananchi wa Tanzania wakiwapo wananchi wa Wilaya ya Chunya wanapata huduma bora na nzuri kwa wakati

Tatu, Taifa linaelekea kwenye kipindi Uchaguzi wa serikali za mitaa niwaombe Wanachunya Wenzangu tujitokeze kujiandikisha na kupiga kura ili kuwachagua viongozi bora kwa maendeleo ya Mtaa, Kijiji na Taifa kwa ujumla ,kwani Tarehe 27 Novemba 2024 ni siku yetu muhimu Wanachunya na Tanzania kwa ujumla ya kuchagua viongozi tuwatakao watakao tuongoza katika misingi ya maendeleo na kulijenga Taifa letu.

*Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,Jitokeze kushiriki Uchaguzi*

# HABARI PICHA



CHUNYA BINGWA WA KUDUMU MCHEZO WA KUVUTA KAMBA (Wanaume) Baada ya kuutwaa ubingwa huo mwaka huu 2024 wakati Halmashauri ya wilaya ya Chunya iliposhiriki mashindano hayo katika viwanja vya Chuo cha Ulimu Butimba kuanzia tarehe 26/8-09/09/2024





Mwenge wa uhuru Wilaya ya Chunya umepokelewa Tarehe 24 Agosti, 2024 na kukimbizwa kilometa 287.4 ambapo miradi yenye thamani ya shilingi Millioni 878,178,764 imezinduliwa, kutembelewa na miradi mingine imeweka Jiwe la Msingi.





*Afisa Utalii Wilaya ya Chunya ndugu Petro Haule akionyesha Fuvu la kichwa cha Tembo lenye taya ya juu na chini, ngozi ya mamba kwa wanafunzi waliotembelea banda la Halmashauri ya Wilaya ya Chunya wakati wa Maonyesho ya nane nane nyanda za juu kusini katika viwanja vya John Mwaakangale Mkoani Mbeya..*



Mkuu wa Mkoa wa Songwe alipotembelea Banda la Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kujionea baadhi ya mazao mbalimbali yanayozalishwa Wilayani chunya.

# CHUNYA

## JARIDA LA MTANDAONI



**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**


S.L.P 73 CHUNYA, MBEYA
SIMU: 025 2520121

www.chunyadc.go.tz
chunyadc_official
@ chunya_official
ded@chunyadc.go.tz


*Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*